**Wikendi ya Maombi ya Ulimwenguni 2024**

viva
together for children

NURU YA ULIMWENGU
Wikendi ya Maombi | 1-2 Juni 2024

## Utangulizi: Vifungu vya Biblia.

Wiki ya maombi duniani inayoandaliwa na viva inawahusu zaidi Watoto kwani uwapa Watoto fursa ya kuomba Mungu na kuwaombea Watoto wenzao. Kauli mbiu kwa mwaka huu wa 2024 ni **'Nuru ya Ulimwengu,'** kuanzia mstari wa 5 wa Yohana 9 pale ambapo Yesu alisema, ", Mimi ni nuru ya ulimwengu." Shabaha kubwa kwenye sura ya 9 ya kitabu cha Yohana, ni uponyaji wa mtu aliyekuwa na upofu.

## Viva ilianzaje?



Wikendi ya Maombi Cambodia 2023

Patrick McDonald, mwaanzilisha wa Viva, anasimulia maono aliokuwa nayo alipokuwa akifanya kazi na shirika moja ndani ya nchi fulani America ya kusini lilokuwa likijishughulisha na maswala ya Watoto wa mitaani . Patrick anasema, aliona picha ya dunia usiku ikizunguka kwa uzuri katka anga yake lakini kwa namna fulani kulikuwa na "giza" mara gafla , miale ya mwanga zikaibuka; ndogo, dhaifu, na isiyo na faida . Baadaye zikaongezeka na kuwa nyingi sana na kuanza kuunganikana kuwa



kama vituo vya mwanga huku zikizunguka eneo fulani. Kwa namna fulani anga ilianza kubadilika kwa kila hatua zilizopokuwa zikiongezeka kuwa imara na kutoa mwanga zaidi. Patrick alijua wazi kuwa maono hayo ni majibu ya Mungu kwake kutokana na maswali ambayo alikuwa nayo, "Ni mpango gani? Kwa jinsi gani, Bwana unatarajia kutimiza matarajio ya Watoto hawa?" Maono hayo yaliwakilisha uhamasishaji mkubwa wa makutano ambayo yalikutanishwa kwa lengo la shughuli moja na kuunganishwa kama mtandao kwa kuwezeshwa kuwa na viwango sawa.

"NURU"

## Rasilimali

Kutokana na simulizi iliopo kwenye kitabu cha Yohana sura ya 9, dondoo hii imefanikiwa kubaini vipengele au jumbe kuu nne, shughuli mbalimbali, mstari wa kumbukumbu na maswali yanayotoa fursa kwa Watoto kuwaongoza Watoto wenzao kwenye maombi. Dondoo hizi za maombi zinajumuisha shuhuda kadhaa zilizotokana na maombi ya miaka ya nyuma, Uhusishwaji, Nyimbo, uwasilishaji kupitia power point na maandalizi ya siku 28 ya maombi yanayopatikana kupitia tovuti ya, www.worldweekendofprayer.com

## Vipengele vinne

i) **Kazi ya Mungu** – Lengo kuu kwa Watoto wadogo.
ii) **Kwa nini kuwa na mashaka?** – Ikijumuisha Watoto wa umri ya kati na chipukizi.
iii) **Yesu ni nani?** – kwa chipukizi.
iv) **Imani ni nini?** – kwa chipukizi na watu wazima.



Wikendi ya Maombi Amerika ya Kusini 2023


Watoto wanaweza kuomba kupitia njia tofauti tofauti: kwa kutengeneza hali ya utatu kipindi cha maombi; kuomba kwa njia ya matawi; kuandika mahitaji ya kuombea kwenye mapulizio ; kuandika maombi kwenye mabango; au kutumia video mbalimbali.

## Mambo ya kuombea (Watoto)

i) Amani na upendo nyumbani na kwenye familia.
ii) Chakula cha kutosha , maji safi ya kunywa , Mavazi, na huduma bora ya afya pale nipatapo changamoto yoyote ya kiafya.
iii) Amani na kupungua kwa matukio ya ukatili dhidi ya Watoto mtaani kwangu.
iv) Kuhusu elimu, kwamba niwe naweza Kwenda shule na kufundishwa na waalimu wema wenye upendo.
v) Ulinzi na usalama dhidi ya wanyanyasaji na walaghai.
vi) Watu wazima wabadilishe fikra zao ili waache tabia ya kuwadharau au kutowajali Watoto.
vii) Makanisa mengi zaidi, kufanya kazi kwa Pamoja katika jiji letu kwa shauku ya kuboresha Maisha na maslahi ya Watoto.

together for children

## 1: Kazi za Mungu.



**Msingi wa Simulizi** Yohana 9:1-12

**Simulizi.**

Siku moja, Yesu alikuwa akitembea Pamoja na wanafunzi wake, gafla wakamuona mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa kwake, akiwa anaombaomba, wanafunzi wa Yesu wakamuuliza Yesu wakisema "Rabbi, ni nani aliye tenda dhambi! Ni mtu huyu au wazazi wake? Ata azaliwe kipofu? Yesu akawajibu na kuwaambia wanauliza swali lisilo sahihi kwani hilo limefanyika ili uweza wa Mungu udhihirike wazi kwa wanadamu. Yesu akasema, "Nikiwa nipo ulimwenguni, Mimi ni nuru ya ulimwengu " Baadaye Yesu alitema mate chini , akatengeneza udongo na kumpaka machoni mtu yule aliyekuwa kipofu na kumwaambia , nenda na uoshe macho yako kwenye Bwawa la siloam. Yule mtu akaenda. Akaosha macho yake. Muujiza ukatokea! Kwa sababu alianza kuona. Ndugu zake na majirani waliokuwa wakimfahamu jinsi alivyo walipokutana naye, walishanga! Na wengine wakawa na mashaka kama kweli muujiza umemtokea. Wakaanza kusema labda ni mtu mwingine ambaye anafanana na yule kipofu aliyekuwa akiombaomba.

Kazi

i) **Sanamu ya udongo** – tengeneza sanamu ya udongo ya mtu mme (Kama vile Yesu). Ikimwaakilisha Yesu ambaye yule mtu kipofu alikutana naye. Alafu ongezea mwanga au kitu chochote kinachowaka kichwani mwake ikionyesha yeye ni nuru ya ulimwengu. Tengeneza sanamu ya mtu mwingine wa pili ikimwaakilisha yule mtu kipofu)

ii) **Ebu jaribu kuigiza , huku ukijifanya kipofu** – kwa kufumba macho jaribu kuchora picha ya mtu aliyekaa karibu na nyumba uone jinsi ilivyo ngumu kuwa kipofu.

### Mstari wa kumbukumbu (A

**Yohana 9:5** Ningali bado ulimwenguni mimi ni nuru ya ulimwengu.'

**Fanya haya** – Jadili maswali haya ili yatoe muongozo kwenye maombi juu ya utendaji Mungu .


i) Mambo mabaya yanapotokea, Mungu anawezaje kuingilia kati na kubadili hali iliojitokeza? Je sehemu yetu ni ipi katika hilo?

ii) Kuna mabadiliko yoyote umeona kwenye familia yako, familia ya rafiki yako, shule au jamii inayokuzunguka? Je tunaweza kuomba juu ya mabadilko zaidi kuendelea kutokea ?

iii) Ilikuwa ni vigumu kwa yule mtu kumwamini Yesu na Kwenda kuosha macho yake kwenye Bwawa la maji. (Angeweza ata kutumia maji yaliyokuwa karibu naye na kuosha uso wake ) Sisi tuna tumaini gani kwa Bwana? Pale ambapo yale ambayo tunaomba kwa Bwana yatachukua muda mrefu? Je tutapambana kwa kadri ya uwezo wetu au tutamsubiria Bwana?

**Shuhuda kutoka Patna India:** Wiki ya maombi duniani mwaka 2023 ilileta utambuzi wenye nguvu kwa Watoto kuhusu wajibu wetu wa kulinda uumbaji mzuri ambao Mungu ametupa. Anjali ni msichana kutoka kituo kimoja cha mafunzo Patna -India, Sasa anawajibika kuzima taa na feni zisizo za lazima, huhifadhi maji kwa kufunga mabomba, miche ya mimea na kuweka mazingira yake safi. Sasa amekuwa shujaa wa asili, mlezi mwenye fahari juu ya uumbaji wa Mungu na mara nyingi huwaimiza ndugu na marafiki zake wajiunge naye.

## 2: Miujiza ya Mungu.



**Msingi wa simulizi** Yohana 9:13-23

Akiisha kuwaambia majirani zake kuwa ni Yesu ndiye aliyemponya , majirani zake wakamchukua na kumpereka kwa mafarisayo. Walipofika kwa mafarisayo yule mtu aliyekuwa kipofu akaelezea kile kilichotokea. Baadhi ya viongozi wakasema, shughuli ya kuchanganya tope kwa ajili ya uponyaji ilifanyika siku ya sabato. Kwa sheria ya wayahudi hakuna shughuli iliyoruhusiwa kufanyika siku ya sabato; Hivyo basi wakakaza kusema mtu anayeitwa Yesu hawezi katoka kwa Mungu kwa sababu yeye ni mwenye dhambi kwa kitendo cha kufanya kazi siku ya sabato, Mafarisayo waliwaita wazazi wa mtu yule ili kuthibitisha kwamba mtu huyo alikuwa mtoto wao na kama alizaliwa kipofu , waliogopa na wakauliza jinsi mtoto wao angeweza kuona sasa. Wale wazazi wa yule mtu wakawaambia mafarisayo wamuulize mhusika mwenyewe kwani ni mtu mzima na anaweza kujieleza vizuri.

**Kazi**

1. **Wafanye Watoto** kuigiza kwa kutumia maneno yao wenyewe na kurudia mara mbili.

2. **Vitovu vya mwanga** – Acha timu za Watoto wachore ramani yenye mtindo wa jiji lao kwenye sehemu kubwa ya kadibodi. Kwenye ramani hiyo watambue mahali shule na kanisa ilipo. Hakikisha sehemu kanisa au shule illipo unafunga taa aina ya LED. Washa taa iwe inatoa mwanga alafu ionyeshwe ikiwakilisha mtandao unaofanya kazi kwa ajili ya Watoto.

### Mstari wa kumbukumbu

**Yohana 9:15b**: "Alinipaka matope machoni," yule mtu akajibu , "nikaosha uso wangu, na sasa naona."

**Utekelezaji:**

Jadilini maswali haya ili yawaongoze kwenye maombi kwa kutambua miujiza ya Mungu.

i. Ina maanisha nini kuwa na mashaka pale ambapo tunamuomba mtu kufanya jambo fulani kwa ajili yetu?

ii. Muujiza ni nini?

iii. Ni wapi tunahitaji muujiza kwa sasa? (Kwenye familia, Shuleni, jamii)

**Shuhuda kutoka kwa Watoto wa Zambia.**

*"Nimejifunza kwamba Mungu aliumba ulimwengu na kila kitu kilichomo, na akawapa watu wajibu wa kuwapenda na kuwatunza Wanyama."*

*"Ombeaneni ninyi kwa ninyi na kumtumaini Bwana. Unaweza kuweka kila jambo mikononi mwa Mungu hata ukiwa na shida Mungu anaweza kukusaidia."*

*"Tunahitajika kutunza uumbaji wa Mungu. Watoto wote wanatakiwa Kwenda shule na kuelimishwa."*

## 3: Yesu, mwana wa Mungu.

**Msingi wa simulizi Yohana 9:24-34**

Baada ya kuwahoji wazazi wa mtu yule kipofu, Mafarisayo walimwiita yule mtu tena na kumwambia "Mpe Mungu utukufu kwa kusema kweli".*Tunajua huyu mtu aitwaye Yesu ni mwenye dhambi* " Akajibu na kuwaambia , "*Awe ni mwenye dhambi au laah!, mimi sijui . Jambo moja ninalojua.!"Nilikuwa sioni ila sasa naona*" Mafarisayo wakamuuliza tena jinsi alivyoponywa. Yule mtu akastaajabu sana kwa nini wanamuuliza uliza swali hilo, na kuwauliza: "*Je nanyi mngetamani kuwa wanafunzi wake?*" Kwa hili Mafarisayo wakamtukana. Baada ya shuhuda nyingi kuhusu Yesu kutoka kwa yule Mtu, Mafarisayo wakamtoa nje ya sinagogi, wakisema wewe ulikuwa umezama katika dhambi tangu kuzaliwa kwako, wathubutuje kutufundisha?"

**Kazi :Nani alisema?** -Wakusanye watoto na uwaweke kwenye mduara kisha uwafumbe macho kwa vitambaa, alafu umchukue mtoto mmoja katikati yao na kumsimamisha katikati ya mduara alafu mwambie aseme " Nenda ukanawe uso kwenye Bwawa la- siloamu" akisha kusema hivyo mwambie ajiunge na wenzake tena kwenye mduara. Akisha jiunge na wenzake, waambie wote watoe vitambaa vilivyofunga macho yao alafu waulize ni nani alichukua nafasi ya Yesu kwa kusema " Nenda ukanawe uso wako kwenye Bwawa la siloamu? Je wanaweza kumtambua kupitia sauti?

### Mstari wa kumbukumbu

**Yohana 9:32-33:** Hakuna mtu aliwahi kusikia Habari za mtu aliyefumbuliwa macho huku alizaliwa akiwa kipofu. Kama mtu huyu hakutoka kwa Mungu , hasingeweza kufanya yote haya.'


**Utekelezaji:**

Jadilini maswali haya ili yawaongoze kwenye maombi kuhusu namna ya kumsikiliza Yesu aliye mwana wa Mungu.

i) Kwa nini Watoto wengine wanafahamu kuwa Yesu ni mwana wa Mungu na wengine hawafahamu?
ii) Ni vitu gani vya muhimu kujua kuhusu Yesu?
iii) Kama maombi ni kuongea na Yesu, Je kwa namna gani tunamsikiliza? Unaweza kumsikiliza Yesu sasa?

**Shuhuda kutoka kwa Asnath, Tanzania.** Asnath ana maika 15 amekuwa akiishi na mama yake tangu pale ndoa kati ya mama yake na baba yake ilipovunjika. Kwenye wiki ya maombi mwaka 2022, alimuomba sana Mungu ili wazazi wake warudiane tena. Mwaka 2023, alinukuliwa akisema,"*Namshukuru Mungu sana kwa namna ambavyo amekuwa akijali haja za watu wake, kwani kwa muda mrefu Baba na Mama yangu walikuwa katika hali ya kutengana kiasi ambacho walikuwa hawawezi kuwasiliana hata kupitia simu ya mkononi ila mara tuu ya kuanza kuwaombea kuna kitu Mungu ameanza kufanya kwani mwisho wa mwaka jana wameanza kufanya mawasiliano kwa njia ya simu. Jambo ambalo linanipa ujasiri wa kuamini kwamba muda si mrefu watarudiana na kuishi Pamoja tena. Utukufu na umrudie Bwana ajibuye maombi yetu*"

## 4: Imani ndani ya Mungu.



**Msingi wa simulizi Yohana 9:35-41**

Yesu alisikia yakwamba Mafarisayo wamemtoa yule mtu aliyekuwa kipofu hapo awali nje ya sinagogi, naye alipomuona akasema, "Je*? Unamwamini mwana wa Adamu?*" ""*Ni nani Bwana?*" Yule mtu akauliza. "*Niambie ili nione kama naweza kumwamini.*" Yesu akamwambia, "*Umemuona hata sasa kwani ndiye anayezungumza nawe;.Ndipo yule mtu akasema*, "*Bwana naamini,*" na akamwaabudu. Kisha Yesu alizungumza kuhusu upofu wa kiroho kwamba baadhi ya watu kama Mafarisayo, hawawezi kuona na kukubali kwamba yeye ni mwana wa Mungu. Wale wasioamini watahukumiwa na kuhesabiwa hatia.

**Shughuli.**

**i)** **Wimbo** – Pata kundi la Watoto au chipukizi kuandaa wimbo wa kawaida.

**ii)** **Kolagi** - Tengeneza kolagi kubwa kwa mabaki ya kitambaa, karatasi ya rangi, au picha za rangi za mambo ambayo Yesu alifanya ambayo yanaonyesha Yeye ni Mwana wa Mungu. Rekebisha hii kwa ukuta. Funika kwa kitambaa cheusi. Watoto huiangazia kwa simu au mienge na kusema, kama walivyofanya Mafarisayo, "Je, sisi pia ni vipofu?" Sasa vua kitambaa cheusi, na nuru inapoangazia mambo ambayo Yesu alifanya, wote husema kwa pamoja, "Yesu alisema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu.

### Msatari wa kumbukumbu

**Yohana 9:38** Na yule mtu akasema "Bwana nasadiki", na akamwaabudu'.

**Utekelezaji:**

Jadilini Maswali haya ili yatoe muongozo namna ya kumuomba Mungu kuhusu Imani ndani ya Mungu.

i) Imani ni nini?

ii) Jinsi gani kuwa na Imani juu ya Yesu, yeye ni nani na anaweza kufanya nini.

iii) Unahisi Yesu anaweza kubadilisha hali nyumbani, hali ya mtaa, mtaa na hata chuo? Je unahitaji Imani zaidi ili uzidi kuamini anaweza kujibu maombi? Kwa nini usiombe afanye hivyo?

**Shuhuda ya mtoto kutoka Cambodia:** Watoto walisema kuna nguvu zaidi katika maombi ya Pamoja. Walizidi kusema walikuwa kama wafalme na malkia pale walipoongoza kundi kubwa la watu kumuomba Mungu. Viongozi wa kanisa walikiri kwamba , wanapaswa kuwafundisha Watoto ambao ndio kizazi kijacho kuwa tayari kwa ajili ya wajibu wao katika utume.

together for children

NURU YA ULIMWENGU

Wikendi ya Maombi | 1-2 Juni 2024

**Maombi ya kuhitimisha:**
Yesu, wewe ni nuru ya ulimwengu. Ulimponya mtu kipofu ambaye hakuwa na uwezo wa kuona tangu kuzaliwa kwake. (Muujiza.); Alilazimika kuwajibika kwa Kwenda kuosha uso wake kwenye Bwawa la siloamu. Alikutumaini. Nisaidie na mimi niweze kukutumaini, Yesu nisaidie nisiwe kipofu wa fikra kama walivyokuwa wale Mafarisayo bali nisaidie kukutumaini na kukutegemea utakapo badilisha hali ya mji wetu ulio katika hali ya umaskini. Washa mwanga wako wa muujiza nyumbani kwangu, mtaani kwangu na shuleni kwangu. Naomba niwe na uhakika

---

together for children

Wikendi ya Maombi duniani ni mpango wa kimataifa wa maombi unaotekelezwa kupitia kampeni inayohamasisha maombi kila wikendi ya kwanza ya mwezi wa sita kila mwaka. Mpango huu ukutanisha mamia kwa maelfu ya watu wazima na Watoto duniani kote kwa ajili ya maombi ambayo uandaliwa chini ya usimamizi wa shirika la hisani la kimataifa linaloitwa Viva kwa kushirikiana na mitandao 38 ya Watoto kutoka nchi mbalimbali duniani. Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya viva ya **www.viva.org**.

Usajili shirika la hisani namba 1053389